# Sauti ya Kweli Kimataifa
## (The Voice of Truth International)

### Toleo la 100

Mzalishaji (Producer):
**World Evangelism Team**

Nakala ya Kiswahili (Swahili copy):
**Swahili Gospel Team**

Mawasiliano:
+255 (0) 764 792 979
+255 (0) 765 098 981

Taarifa (Notice):

Kitabu hiki hakiuzwi, kinatolewa bure na kanisa la Kristo kupitia taasisi ya ***World Evangelism Team (WET).***

This book is not for sale, it is freely given by the church of Christ throuth the institution ***World Evangelism Team (WET).***

# Dibaji

Kitabu hiki kimetayarishwa katika mtindo wa jarida lenye makala mbalimbali za kidini kutoka kwa waandishi tofauti tofauti. Makala hizo zinafundisha kuhusu Mungu, Ushahidi wa Neno, Nguvu ya Neno, Wokovu, Kanisa, Mafundisho ya kuyaishi, Matendo ya Kikristo, Ibada, Maisha ya Kikristo, Nyumba ya Kikristo, Masomo katika vifungu, Wahusika mbalimbali katika Biblia, Maswali yanayojitokeza katika Biblia na, Hotuba. Yote haya yameundwa mahususi ili kumwezesha msomaji kupata elimu ya Biblia katika mada mbalimbali. Hali kadhalika kitabu hiki kitakusaidia kujenga, kukuza na kuimarisha imani yako katika Kristo.

Vitabu hivi vipo katika mtiririko wa matoleo ambapo matoleo kwa lugha ya Kiswahili yameanza na toleo la 90. Matoleo haya hutoka mara tatu kwa mwaka. Mara baada ya uchapishaji wa vitabu hivi hufuatiwa na usambazaji katika nchi za Afrika Mashariki palipo na wazungumzaji wa Kiswahili.

Vitabu hivi kwa sasa vinapatikana katika lugha za Kiswahili, Kiingereza, Kihindi, Paite, Tamil na, Telugu. Na kusambazwa katika maeneo mbalimbali duniani.

Kazi kubwa inafanyika katika uandaaji wa vitabu hivi. Pesa na muda mwingi ni sehemu ya ufanikishaji wa huduma hii. Watenda kazi wanaojitolea, nchini Marekani, Tanzania na maeneo mengine wanafanya kila linalowezekana kuhakikisha huduma hii inaendelea kuwepo kwa ajili ya manufaa ya kanisa na watu wa Mungu katika siku za leo na baadaye.

Licha ya kazi na gharama zote hizo, bado vitabu hivi vinatolewa bure na kwa upendo mkubwa kwa kila mtu apendaye kujifunza Neno la Mungu. Hivyo, tafadhali tunakuomba uthamini kazi hii kwa kujifunza wewe binafsi, na kukihifadhi vizuri kitabu chako ili kiwasaidie na wengine. Zaidi sana, tutafurahi ikiwa utatumia maarifa unayoyapata kutoka katika kitabu hiki na kuwafundisha wengine. Hilo ndilo lengo hasa!

## CHAGUO LA KANISA LA KRISTO…

**SIO HATA KIFO AMBACHO KINGEWEZA KUMZUIA KRISTO ASIANZISHE KANISA LAKE** (Mathayo 16:18-19) NA HALIWEZI KUANGAMIZWA (Waebrania 12:28).

**…SI MADHEHEBU:** Kanisa la Bwana lilianzishwa katika siku ya Pentekoste (Matendo 2). Hata madhehebu kongwe ni changa mno kulinganisha na Kanisa moja la KWELI aliloliahidi Kristo na kulianzisha (Mt. 16:18). Watu watakwambia ujiunge na kanisa ulipendalo. Yesu hajaidhinisha hilo. Ni Bwana pekee ndiye mwenye mamlaka ya kuziingiza roho katika kanisa lake. Ni wale tu wnaolipokea Neno kwa furaha, kubatizwa na kuokoka (Mdo 2:41, 47; Mk. 16:15-16)

**…NI UFALME WA KRISTO:** Ulianzishwa katika siku ileile na eneo lilelile (Isa. 2:2-3; Mdo. 2:1-47). Sifa za kuingia katika ufalme na kanisa ni zilezile; ufalme (Yn. 3:3-5), kanisa (Mdo. 2:38-47). Chakula cha Bwana ni kilekile katika ufalme (Mt. 26:29) na kanisa (1 Kor. 11:20-27). Utukufu wa ufalme (Isa. 2:2) ndio utukufu wa kanisa (Efe. 3:21). Muda wa ufalme (1 Kor. 15:24) ndio muda wa kanisa (1 The. 4:16-17).

**…MISINGI:** Yesu alilinunua kanisa kwa damu yake (Mdo. 20:28). Je, mwanadamu anathubutuje kusema, "haijalishi ni kanisa gani!" haijalishi mtu ni mshirika wa madhehebu gani, makanisa yote ya wanadamu na mafundisho ya wanadamu yatang'olewa na kuangamizwa (Mt. 15:13).

**…FUATISHA KIELELEZO CHA KANISA KAMA ILIVYOTAJWA KATIKA MAANDIKO** (1 Tim. 1:13; Tit. 1:9; 1 The. 5:21).

**KWA KUFUNDISHA** (2 Tim. 4:1-4)
**KWA UONGOZI** (1 Tim. 3:1-13; Tit. 1:5-9; Flp. 1:1)
**KWA KUISHI** (Flp. 1:27; 1 The. 4:1-12)
**IBADA** (Yn. 4:23-24; Mdo 2:42; Kol. 3:16-17; 1 Kor. 16:1-2)
**MAONYO** (Rum. 16:17-18; 1 Tim. 6:3; Ufu. 22:18-19)

**…KUMWABUDU MUNGU KATIKA ROHO NA KWELI:** (Yn. 4:23-24) Mt. 15:8-13; Mdo. 2:42; Kol. 3:16-17; 1 Kor. 16:1-2

**…LITAOKOLEWA NA YEYE**: Efe. 5:23 inafundisha kwamba Yesu ndiye Mwokozi wa mwili (kanisa Efe. 1:22-23). Ikiwa mtu hayupo ndani ya kanisa lake, basi hawezi kuokolewa na Yesu. Angalia pia katika 1 Pet. 1:3-5

**JE! WEWE NI MSHIRIKA WA KANISA LA KRISTO?**

**Robert C**




# MCHORO WA KUPULIZIA!

**Louis Rushmore**

Maana ya msingi ya "kujisitiri" (1 Timotheo 2:9) ni kuwa katika "utaratibu" au "kujipamba." Ndiyo, halafu, kujisitiri kunajumuisha yote mawili kutovaa vizuri vivyo hivyo na kuvaa kulikopitiliza. Kulingana na kujisitiri kama inavyohusiana na uvaaji, **vazi hapo mwanzo** lililetwa kwa makusudi mawili, **kuficha umbo la mwanadamu** na **kumlinda** mtu dhidi ya **viatarishi vidogo vidogo** (Mwanzo 3:7, 21). Mungu aliwabadilishia Adamu na Hawa mavazi ya majani ya mtini na kuwavika kwa ngozi ya mnyama. Nguo kama hizo, bila kujali nyenzo ambazo zilitengenezewa, kawaida huwa ndefu kutoka kwenye mabega hadi kwenye vifundo vya miguuni. Mungu aliamua katika Bustani ya Edeni kwamba vazi la kujisitiri litakuwa la namna gani kwa wanaume na wanawake.

Mara nyingi siku hizi, hata hivyo, nguo hazifichi umbo la mwanadamu wala hazimkingi mtu kutokana na hali ya hewa. Umbo la mwanadamu linapokuwa halijafichwa, ngozi kwa kiasi kikubwa huwa wazi au unakuta mavazi yamejichora katika mwili wa mtu, uvaaji huo ni kinyume na makusudi ya awali ya uvaaji, na huko si kujisitiri. 1 Wakorintho 12:23 inaonesha kwamba watoto wa Mungu watajisitiri kwa kufunika **"viungo vyao vya siri."**

Kwa miongo kadhaa, mavazi yanayovaliwa hadharani na watu wengi na hata Wakristo, yamekuwa yakifunua kulingana na kujisitiri

kunakozungumziwa na Biblia. Nguo za kubana, magauni mafupi, sketi fupi na kaptula, magauni ya kupitisha mwanga, nguo za ufukweni n.k, si kujisitiri kibiblia. Hakuna mtu anayetakiwa kuvaa mavazi hayo hadharani na hususani Wakristo kamwe hawapaswi kutambuliwa kwa uvaaji huo husio wa kujisitiri.

Kwa sehemu kubwa leo hii, nguo nyingi zinazochaguliwa na wengi, kwa bahati mbaya hata na Wakristo walio wengi, **kibiblia si mavazi ya kujisitiri mbele za watu**. Ukiongezea mifano ya kutovaa vizuri hapo juu, wanawake wanavaa nguo zinazofanana na hizo, ambazo hung'ang'ania vizuri mwili wa mwanadamu. Hakika hakuna kinachoachwa kwenye mawazo! Wazazi wanawezaje kuwa wavivu wa kuelewa na kujali, kuhusu mafundisho ya Biblia pamoja na mienendo ya tamaa mbaya, kuwaruhusu watoto wao kuwa na utovu wa nidhamu kiasi hicho? Enyi waume, kwa nini mnawaacha wake zenu waende hadharani wakiwa wamevaa bila staha?

Je, unakubaliana na ufafanuzi wa nani kuhusu “kujisitiri” au kuvaa kunakokubalika? Kama mume au baba, je, unamruhusu mkeo na watoto wako kuvaa vazi la majani ya mtini walilovaa Adamu na Hawa, au unasisitiza kwamba familia yako wavalie vazi la staha linalofafanuliwa na Mungu? **Je, ni mbunifu yupi wa mavazi ambaye familia yako inampendelea, Mungu au Shetani?** Je, kuna tofauti gani leo hii baina ya mavazi ya kujisitiri na ***“mavazi ya kikahaba”*** (Mithali 7:10)?

## JE, VAZI LA KUJISITIRI NI LIPI?

Shadrack S. Msambaza

Ni ukweli usiopingika kwamba, kila utamaduni una vazi lake la asili. Na ikiwa vazi hilo linakubalika na utamaduni huo, basi vazi hilo ni sawa. Lakini kwa sababu tu vazi fulani la asili linakubalika na jamii fulani haimaanishi kuwa vazi hilo ni la kujisitiri. Vazi la kujisitiri linapaswa kuwa ni vazi ambalo kimaadili litakubalika na jamii zote za dunia.

# Nami Nikiinuliwa Juu!

Jerry Bates



Katika Yohana 12:32-33, Yesu aliwaambia wanafunzi wake baadhi ya mambo ya kushangaza na maneno ya hajabu. ***"Nami nikiinuliwa juu ya nchi, nitawavuta wote kwangu. Aliyanena hayo akionyesha ni mauti gani atakayokufa."*** Neno la Kiyunani la "kuinuliwa juu" linamaanisha kutukuzwa. Limetumika mara kadhaa katika Agano Jipya, wakati wote likirejelea kusulibiwa kwa Kristo. Hata hivyo, nadhani ni salama zaidi kusema kwamba utukufu wa Kristo wa baadaye ulipatikana katika kufufuka na kupaa kwake pia imejumuishwa katika neno hili. Waliokuwa wakimsikiliza Yesu hawakuweza kuelewa fundisho hili. Walijua Maandiko yalifundisha kwamba Masihi na ufalme wake ungekuwa wa milele. Kwa kuwa walidhani ufalme huo ni wa kidunia, hivyo, hilo lilimaanisha kwamba Masihi asingeweza kufa. Lakini pia, walielewa vizuri sana kuwa Yesu alikuwa akiongelea kifo chake. Kwa kweli walishindwa kujua wakamate lipi kati ya mambo hayo mawili.


Katika aya hizi tunaona mambo matatu ya kushangaza, ambayo kwa ujumla wake ulimwengu huwa hauyaelewi. Kwanza kabisa, tunaona kwamba msalaba unamaanisha hukumu ya ulimwengu (12:31). Katika akili ya watu wengi, msalaba umeleta wokovu, lakini Yesu alisema kwamba msalaba ungeleta hukumu.

Wengi wana amini kwamba kwa kuwa Yesu alikufa msalabani kwa ajili yetu, basi Mungu hata mtupa mtu yeyote motoni. Hivyo, ulimwengu ulidhani kuwa kitendo hicho kilimaanisha hukumu hiyo ilipitishwa kwa Yesu pale msalabani, lakini kihalisia msalaba pia uliwaleta wao hukumuni. Kwa kuzingatia mitazamo hii, inawezekanaje kusema kwamba msalaba ulileta hukumu?

Nuru ni hukumu dhidi ya giza. ***"Na hii ndiyo hukumu; ya kuwa nuru imekuja ulimwenguni, na watu wakapenda giza kuliko nuru; kwa maana matendo yao yalikuwa maovu. Maana kila mtu atendaye mabaya huichukia nuru, wala haji kwenye nuru, matendo yake yasije yakakemewa. Bali yeye aitendaye kweli huja kwenye nuru, ili matendo yake yaonekane wazi ya kuwa yametendwa katika Mungu."*** (Yohana 3:19-21). Kwa ulimwengu kumkataa Yesu kumefunua asili yake na kumefunua kwamba ni nani aliyeupande wa Mungu. Kumkataa kwake Yesu kulionesha kwamba hawakustahili kupata uzima wa milele pamoja na Mungu. Baadaye katika sura hii, Yesu alisema kwamba yupo mhukumu wa ulimwengu huu (12:48), na hakimu huyo ni maneno ya Yesu. Pindi ulimwengu ulipomkataa Yesu, walikataa njia ya wokovu. Hivyo, wakati ambapo msalaba unaleta wokovu kwa wale wanaoyakubali maneno ya Yesu, pia wakati huohuo unaleta hukumu kwa wale wanaomkataa Yesu.

Pili, Yesu alisema msalaba unamaanisha kushindwa kwa "mtawala wa ulimwengu huu" (12:31). Mtawala wa ulimwengu huu ni Shetani. Maadui wa Yesu kwa muda mrefu walipanga njama ya kifo chake, na walidhani kwamba kifo chake ni ushindi wao mkubwa. Walibeza wazo la kwamba hatia yoyote inayotokana na kifo cha Yesu ingewafikia wao. Kwa ujasiri walipaza sauti, *"msulibishe,"* na pia kwa hiari walikubali hatia yoyote itokanayo na kifo chake wakisema, *"damu yake na iwe juu yetu na juu ya watoto wetu,"* Ibilisi na wafuasi wake walitaka kumwangamiza Yesu, lakini msalaba ilikuwa ni hatua ya kwanza ya kutukuzwa kwake kama Mtawala na Hakimu juu ya vyote na wote.

Kifo cha Yesu kilitokea kuwa ni ushindi dhidi ya Shetani na wafuasi wake, ilikuwa ni pigo. Kwa kifo chake, Yesu aliangamiza nguvu za Shetani. Kufufka kwake kuliangamiza nguvu za kaburi na kamba za kifo (1 Wakorintho 15:54-57). Pia kifo cha Yesu kinatuwezesha kumshinda Shetani. Yohana alisema, ***"Nikamwambia, Bwana wangu, wajua wewe. Akaniambia, Hao ndio wanatoka katika dhiki ile iliyo kuu, nao wamefua mavazi yao, na kuyafanya meupe katika damu ya Mwana-Kondoo."*** (Ufunuo 7:14). ***"Nao wakamshinda kwa damu ya Mwana-Kondoo, na kwa neno la ushuhuda wao; ambao hawakupenda maisha yao hata kufa."*** (Ufunuo 12:11).



Mwishowe, tunaona kwamba msalaba ulimwezesha Yesu "kuwavuta watu wote" kwake (12:32). Tazama kwamba Yesu alisema kwamba ni kwa njia ya msalaba ambayo Mungu angeitumia kuwavuta watu wote kwake. Kwamba ni Kristo ambaye angewavuta watu wote. Hii haieleweki kwa ulimwengu. Walimu wa ulimwengu kamwe wasingeweza kutumia mateso kuwavuta watu kwa Mungu. Wengi wangefikiri kwamba ili uwavute watu kwa Mungu, basi anatakiwa mtu atoe zawadi. Kwa kweli, wakati Yesu akiwepo duniani, wengi walimfuata wakitumai kupata faida za mali. Wengine

walimfuata ili wafurahie chakula ambacho angewapa kwa mwujiza. Wengine walimfuata ili tu waone miujiza mikubwa. Wayahudi wengi walimtarajia Yesu awe mfalme wa kidunia, kwa hiyo wangepata faida ya kuwa chini ya ya mfalme mkuu mwenye nguvu. Pindi walipogundua kwamba Yesu hatawapa haya yote, walimwacha wakaondoka.

Yesu alisema kwamba angewavuta watu kwa njia ya msalaba, ambayo kwa hiyo anaonesha upendo wake mkuu kwa ulimwengu. Huu ni upendo ambao hatuwezi kuuelewa vikamilifu. ***"Kwa maana hapo tulipokuwa hatuna nguvu, wakati ulipotimia, Kristo alikufa kwa ajili ya waovu. Kwa kuwa ni shida mtu kufa kwa ajili ya mtu mwenye haki; lakini yawezekana mtu kuthubutu kufa kwa ajili ya mtu aliye mwema."*** (Warumi 5:6-7). Mwanadamu hawezi kufa kwa ajili ya adui zake, lakini hicho ndicho haswa alichokifanya Yesu. Yesu alikufa kwa ajili yetu wakati tulipokuwa tumepotea katika dhambi, wakati tulipokuwa adui wa Mungu. Tunapotambua kina cha upendo wa Mungu, inapaswa tuwe na hamasa ya kuyatoa maisha yetu kwake. Kwa nini tusitake kumgeukia Mfalme mwenye upendo namna hiyo?

Zaidi sana, Yesu alisema kuwa atawavuta watu wote kwake. Hii haimaanishi kuwa wamepangiwa hivyo bila hiari yao, lakini inamaanisha kwamba watu wote bila kubagua, Wayahudi au Mataifa, wote wanaweza kupokea wokovu. Hakuna ubaguzi wa rangi wala vikwazo vingine vya kumwendea Mungu. Kifo cha Yesu kiliangamiza vizuizi vyote ambavyo vilimtenga mwanadamu na Mungu na wanadamu kwa wanadamu. Sasa tunaweza kuwa na ushirika mmoja pamoja na Mungu, na sisi kwa sisi (1 Yohana 1:7). Husikubali kifo cha Yesu kiwe cha bure tu maishani mwako. Kama tutayakataa maneno ya Yesu, basi tunafanya kifo chake kutokuwa na faida, na kwa hiyo tunazihukumu wenyewe nafsi zetu kuelekea utengano wa milele mbali na Mungu.



1932-2008

# Kutazama Nyuma

J.C. Choate

Imekuwa takribani miaka 2,000 tangu Kristo awepo na kufa juu ya msalaba ambao kwa huo tunaweza kuokolewa na kuwa na tumaini la uzima wa milele. Aliahidi kulijenga kanisa lake, na kupitia mitume, kanisa lilianza katika mji wa Yerusalemu katika mwaka wa 33 B.K. Lilipewa **agizo kuu,** ambalo lilihusu dunia nzima, na hata kila mtu katika ulimwengu wote (Mathayo 28:19-20; Marko 16:15-16). Mpango ulikuwa ni kuhubiri habari njema za wokovu katika mji wa Yerusalemu, kisha katika Yudea, Samaria na hatimaye mpaka mwisho wa dunia (Matendo 1:8). Wakiwa na ahadi ya Bwana kuwa pamoja nao (Mathayo 28:20), na kwa uongozi wa Roho Mtakatifu, mitume na waongofu wapya walifuata mpango huo. Ndani kizazi hicho, walihubiri Injili kwa kila kiumbe chini ya mbingu (Wakolosai 1:23). Tena, tunasoma maneno ya mtume Paulo, pale aliposema, ***" Lakini nasema, Je! Wao hawakusikia? Naam, wamesikia, Sauti yao imeenea duniani mwote, Na maneno yao hata miisho ya ulimwengu."*** (Warumi 10:18).

Tangu wakati huo ulimwengu haujawahi kuwa vilevile. Adui alimnenea Paulo na Sila kuwa **wameugeuza ulimwengu juu chini** kwa mambo waliyokuwa wakiyahubiri (Matendo 17:6). Kwa kweli, walimhubiri Kristo kama Bwana aliyefufuka, na kwa njia ya imani katika Yeye na kumtii, maisha yalibadilishwa, na ulimwengu wa tofauti ukawekwa katika mwendo. Ingawa, kwa vile tunavyojua, Injili haijapelekwa tena katika ulimwengu wote tangu wakati huo hadi leo, lakini bado imeacha athari katika kizazi cha mwanadamu

kwamba mageuzi hayo bado yapo hata leo. maadili, sheria, nafasi za wanawake, familia, mahusiano ya kiutu, maadili ya kazi, siasa, mifumo ya kimahakama, elimu, sanaa, muziki na mtazamo wa utumwa, vita na dhambi umebadilika. **Vyovyote ulimwengu uwezavyo kuwa mbaya, bado utabaki kuwa mzuri kama ulivyo kwa sababu ya Kristo na Injili.**

Kwa upande mwingine, licha ya mafanikio ya ulimwengu, urefu tunaoweza kuufikia katika uchumi wetu, magari, teknolojia, mawasiliano na uzalishaji, bado kama wanadamu, mtu si chochote pasipo Bwana. Kama tunaweza kufanya haya yote sisi wenyewe, fikiri kile ambacho ubinadamu unaweza kufanya katika kumtii Mungu! Kumkana Muumba wetu hakutakwenda kubadili ukweli kwamba Mungu yupo. Kumkataa Yesu na Ukristo hakutaupeleka ubinadamu katika kilele, bali isipokuwa kutamshusha katika viwango vya chini vya uwepo na kuwa "wanyama" kama wanasayansi wanavyodai kuwa mwanadamu ametokea katika mnyama.

*Lakini fikiri kwamba ingekuwaje kama kila kizazi cha Wakristo kingeendelea kuipeleka Injili kwa kila kiumbe tangu wakati huo mpaka wakati wa sasa!* Vita vingi vingekomeshwa. Dhambi nyingi zisingepata umaarufu na kukubaliwa kama ilivyo sasa. Taswira yote ya ubinadamu ingekuwa shwari nay a utauwa. Hata hivyo, vizazi vilivyofuata havikutii agizo lao, na tunaposhindwa kufanya mapenzi ya Mungu, tunapata tabu. Ulimwengu wote sasa unalipia kwa majanga mazito, na huuu ni mwanzo tu labda tuamke na kumrudia Bwana katika utii.

Ni aibu gani kufikiri kwamba tumekuwa na vifaa vyote katika kalakana yetu vifaa vya kuhubiria ulimwengu na vya kutunzia wokovu wetu wenyewe katika mchakato huo, lakini bado hatujavitumia. Matokeo yake, Wakristo wengi wanakaa tu, katika ujinga wa kiroho, wakikataa ukweli wa Biblia, wakishirikiana na makosa ya watu wa kidini na kuishi kama ulimwengu ulivyo. Hili ni anguko letu wenyewe, la familia zetu na ubinadamu. Kanisa halikui;

watu wa Bwana wenyewe wanakataa baraka zote ambazo tungezipata kama tungefanya kazi ambayo Bwana wetu aliyotuagiza kuifanya. Pia tumezikataa kupeleka Injili na uponyaji wa nguvu zake katika baadhi ya maeneo ya dunia.

Ndiyo, tunapoyatafakari mambo haya, tunaweza kuhuzunika juu ya yale ambayo yangeweza kuwa, lakini tupo hapa tulipo kwa sababu ya kutokufanya ipasavyo! Tunaishi katika udhaifu kufikia kukata tamaa na kuhisi kwamba hakuna chochote kitakachokuwa sawa, lakini, badala yake, na tutambua makosa yetu na tusimame wima tukiwa na dhamila kwamba, mwishowe tutamtii Bwana na kufanya uinjilisti duniani!bado tunaweza kufanya hivyo. Hilo ndilo tumaini letu na tumaini la wanadamu kwa leo, kesho na milele.

# Tugange ya Mbele

Inafurahisha kuishi katika karne moja na sasa kuona karne nyingine ikiingia! Kanisa la karne ya 20, tumeona tukipata na kupoteza. Makosa mengi yalifanywa, na cha kusikitisha zaidi, hatukunyanyuka katika eneo la kuuhubiri ulimwengu.

Hatuwezi kufikiri jinsi ambavyo hali ingekuwa, lakini ni lazima tuchukue nia ya mtume Paulo pale aliposema, ***"Ndugu, sijidhanii nafsi yangu kwamba nimekwisha kushika; ila natenda neno moja tu; nikiyasahau yaliyo nyuma, nikiyachuchumilia yaliyo mbele; nakaza mwendo, niifikilie mede ya thawabu ya mwito mkuu wa Mungu katika Kristo Yesu"*** (Wafilipi 3:13-14).

Sasa tupo kwenye karne ya 21, na tunazamia kuwa na tumaini na matarajio makubwa. Yesu aliwaagiza watu wake, kanisa, waende ulimwenguni pote wakahubiri Injili kwa kila kiumbe (Marko 16:15-16). Pia aliahidi kuwa panoja nasi na kutusaidia kufanikisha kazi hii (Mathayo 28:19-20). Lengo letu ni lazima liwe kumtii Yeye, tukiziweka akili zetu katika dhamira ya mapambano. Tunaweza kuwa uhakika kwamba hawezi kutuagiza kitu ambacho anajua kuwa hatuwezi kukifanya. Kwa hiyo, tunaweza kusonga mbele kwa ujasiri. Pia tunajua kwamba tuna ujumbe mkuu kuliko yote ulimwenguni,

**habari njema kwamba Yesu alikufa ili tuweze kuokolewa na kuwa tumaini la uzima wa milele.** Itawabadilisha wanawake kwa wanaume, familia, nchi na ulimwengu. Ulimwengu ambao umejaa machafuko ya kuumiza, na kwa hayo tuhamasike kufanya kazi!

Kwa msaada huo, tunawezaje kushindwa? Kuna sababu nyingi kwa nini tunaweza kufikia lengo lake:

- **Kanisa** linapatikana ulimwenguni pote. Ingawa, tukikiri, tupo wachache kwa idadi ukilinganisha na idadi ya kubwa ya watu waliopo duniani, lakini bado kuna idadi inayoridhisha ya Wakristo wanaoweza kuendeleza agizo hili kuu.
- Makanisa hayako katika "uchanga" wao katika nchi hizi za mbali, lakini yanajumuisha Wakristo wa kizazi cha pili na cha tatu katika matukio mengi. Hii ina maana kwamba kuna ukomavu wa kiroho unaowawezesha ndugu wenyeji katika “mashamba ya utumishi” kuinjilisha katika miji na vijiji jirani.
- Kuna shule za Biblia, machapisho, vipindi vya redio na TV katika mataifa haya mengi, vinavyowawezesha Wakristo wa huko kufuatilia mafundisho yaInjili katika vyombo vya habari.
- Pia tuna Wakristo kote ulimwenguni ambao wameelimishwa katika lugha ya Kiingereza, na katika lugha zao wenyewe, ili kuwezesha utafsiri wa nyenzo ufanyike kwa usahihi.
- Kuna aina nyingi za usafiri, zinazowawezesha Wakristo kufika kwa haraka kule wanapoenda. Tumebarikiwa sana kuwa na ndege zinazozunguka ulimwengu kwa muda wa saa chache. Ndani ya nchi, kuna magari, mabasi na gari-moshi, na menngi yao yanapatikana kila mahali.
- Tunapitia mapinduzi makubwa zaidi ya mawasiliano yanayojulikana na mwanadamu. Wakati redio, TV, mfumo wa kebo, satelaiti, simu, kinasa sauti, mashine za uchapishaji, mfumo wa posta, faksi, intaneti, Facebook, YouTube na vifaa vingine kama hivyo vinaweza kusaidia ulimwengu wa kimwili kufikisha ujumbe wake, sisi kama Watu wa Bwana tunaweza pia kutumia njia hizi zote kufikisha Injili katika mataifa kwa haraka. Uwezekano usio na

mwisho upo, na daima tunahitaji kutafuta njia ambazo tunaweza kuzitumia kwa ufanisi zaidi kwa ajili ya kuendeleza kazi ya Bwana.

- Hatimaye, kuna amani ya wastani duniani kote ambayo inafanya uinjilisti kuwa salama katika mataifa mengi. Hata mahali ambapo kuna vita na mizozo ya ndani, hizi zinaweza kuwa zana zenye nguvu za kufungua milango ambayo kwa kawaida ingekuwa imefungwa.
- Kutokwenda pamoja na ulimwengu wa kidini na mafundisho ya wanadamu kunaweza kuleta vikwazo, lakini kwa upande mwingine, kuhubiri upendo, umoja wa kanisa, umoja wa waumini wote, kuvaa jina la Bwana na kubaki katika Biblia katika masomo yote.. Hakika, hatuwezi kuiboresha Injili zaidi ya ilivyotolewa kwa uvuvio wa Roho Mtakatifu.

Inaweza kubishaniwa kuwa sasa kuna zaidi ya watu bilioni 7 duniani, huku matarajio ya idadi hiyo ikiongezeka maradufu ndani ya miaka michache. Wenye mioyo dhaifu wanaweza kuuliza, "Inawezekanaje kwa kanisa dogo la Bwana kuhubiri idadi kama hii?" Hata hivyo, subiri kidogo! Tayari tumeona zana kubwa sana ambazo Mungu ametoa, kupitia wakati Wake wa majaliwa. Je, hatuwezi kutambua kwamba Alijua ni watu wangapi wangekuwa ulimwenguni leo hii na ni zana gani zingehitajika ili kuwafikia? Ametoa kwa wingi kila kitu kinachohitajika kwa ajili ya kuwafundisha watu wote duniani leo, na tunaweza kuwa na uhakika kwamba kadiri idadi ya watu inavyoongezeka maradufu na mara tatu, au vyovyote vile, Mungu ataendelea kuandaa njia ambayo kwayo Injili inaweza kuifikia kila nafsi. Hata kwa wakati huu huu, inawezekana kuwafikia watu wengi zaidi duniani kwa mahubiri moja kupitia satelaiti! Swali ni je, tunataka kuhubiri mahubiri hayo ya kutosha na kuweka lengo la kuwafikia?

Hatupaswi kumdharau Bwana na watu wake na kile tunachoweza kufanya. Jambo la kuhuzunisha ni kwamba, kwa sehemu kubwa, tumeruhusu wengine kutumia njia hizi kuu za mawasiliano, wakati kwa hakika Mungu amezitoa kwa ajili ya

matumizi ya watu wake mwenyewe katika kueneza Injili ulimwenguni! Tunangoja nini? Kwa nini usishike zana hizi ulizopewa na Mungu na kufanya haraka kutekeleza Agizo Lake Kuu?

Fikiri kuhusu hili pia. Tunapohubiri Injili, zaidi na zaidi watu watamtii Bwana ili kuwe na watenda kazi wengi zaidi wa kufanya kazi na fedha zaidi za kulipa gharama zinazohusika zitapatikana. Unawezaje kushinda hilo?

Kuna mimbari, kazi binafsi, fasihi, mahubiri ya redio na TV, shule, vituo vya wanafunzi, kazi ya kutoa msaada wakati wa misiba, misaada kwa maskini, na njia nyingine nyingi za kufundisha na kushawishi watu kwa ajili ya Bwana. Tunahitaji kutafuta njia zozote za kuwafikia waliopotea, na tunahitaji kuzitumia kwa bidii.

Kadiri tunavyofanya zaidi, bila shaka, na kadiri wale naofundishwa wanaongoka, ndivyo tutakavyokuwa na upinzani kutoka kwa ulimwengu, hata kutoka kwa ulimwengu wa kidini. Hata hivyo, upinzani na mateso yataleta utangazaji, yatasaidia wengine kulijua kanisa na kazi yake, watajifunza ujumbe wake na kuunda hamu katika mioyo ya uaminifu ya kumtii Bwana na kuwa sehemu ya kazi Yake kuu. Hili ndilo lililotokea katika karne ya kwanza kulingana na Maandiko ya Agano Jipya, na hali hiyo hiyo itafuata katika karne yote ya 21 tunapomweka Bwana kwanza katika maisha yetu na kuuhubiri ulimwengu.

Ah! Ni furaha iliyoje kumtii Mungu, kuokolewa, kumwabudu, kumfuata na kumtumikia, na kuona mapenzi yake yakitimizwa! Kama watoto Wake, tunatazamia miaka ijayo na yote ambapo tutaweza kufanikisha mpango pamoja Naye. Hii itatubadilisha, na itabadilisha ulimwengu. **Pamoja na Kristo, tunatarajia ushindi. Pamoja na Kristo, kutakuwa na ushindi!**

## HIVI, TUNAFUATA MPANGO?

**Shadrack S. Msambaza**

Mpango mkakati wa Mungu wa kuhubiri Injili ni huu:

1. Wazo KUU: **"Mataifa yote wawe wanafunzi"** (Mt. 28:19-20)
2. Hatua za kufikia Wazo Kuu (Matendo 1:8):
    a. "Yerusalemu," = Anza ulipo.
    b. "Uyahudi wote," = Kisha maeneo jirani.
    c. "Samaria," = Kisha nchi ya jirani.
    d. "Mwisho wa nchi" = Hatimaye mataifa mengine.

# YALIYOMO


Mchoro wa Kupulizia!....................4

Nami Nikiinuliwa Juu!....................6

Kutazama Nyuma....................10

Kristo ni Mwokozi wa Mwili....................19

Je! Uliuliza Swali Lolote Zuri Leo?....................22

Maneno Saba ya Mwisho....................23

Mtu Anayesimama Katikati....................25

Zaburi 119....................27

Tunoe Mashoka Yetu....................29

Tuirudie Biblia ili Tuwe Wamoja....................30

Kama Uliokoka Kabla ya Ubatizo....................32

Farasi wa Sauli (wa Tarso) Alikuwa na Rangi Gani?....................34

Wale Walio Tayari…....................36

Ubatizo, Nini Mtindo Wake?....................38

Kabla ya Madhehebu....................43

Maneno Ambayo Kanisa la....................45

Bwana Huitwa katika Biblia....................45

Kujenga Imani:....................48

Vilivyokithiri Huzaa Vilivyokithiri....................53

Kumbuka Wewe ni wa NANI....................56

Mkinipenda....................59

Sehemu Ya Uponyaji....................61

Uanaume Wenye Sumu....................................................................63
Je! Mungu Anasema Nini Kuhusu Kulea Watoto?..............................64
Mabenchi Tupu..............................................................................66
Kuponya Huzuni.............................................................................68
Ndoa Zisizo na Furaha ...................................................................73
Si Kosa la Mungu............................................................................73
Usiwazuie Watoto Wadogo.............................................................75
Utakaso Wa Kimungu Wa Siku Ya Saba...........................................78
Kutohoa Au Kutafsiri.......................................................................81
Mungu Alikuwa Wapi Wakati Stefano Alipomwitaji? ......................85
Kuwa Barnaba...............................................................................87
Mbingu Mpya na Nchi Mpya ..........................................................89
Je! Kuna Waliookoka Katika Makanisa Yote?..................................91
Historia ya Urejesho ......................................................................93

**MAKALA NA VIJAZI**

Chaguo la Kanisa la Kristo......................................................................03
Nasaha za Msambaza..........................................................5,15,60,80,94
Dakika 5 za Kujifunza Biblia....................................................................18
Je, Ulijua?.................................................................................................24
Rubi za Robison...................................................................................28, 92
Hotuba ya David.......................................................................................31
Tafuta Aya.................................................................................................41
Tafuta katika Biblia....................................................................................47
Maoni ya Haraka.......................................................................................55
Je, Unapimaje?.........................................................................................62
Sarafu za Kenny........................................................................................74
Msaka Tonge.............................................................................................84



# Dakika 5 Za Kujifunza Biblia

## Ufalme wa Yesu Kristo Bwana Wetu

**Paula Bates**

1. Akawaambia, Amin, nawaambia, Pana_____ katika hawa wasimamao hapa, ambao hawataonja_____ kabisa, hata watakapouona______wa Mungu umekuja kwa nguvu. (Marko 9:1)
2. Naye alituokoa katika nguvu za giza, akatuhamisha na________katika ufalme wa________wa pendo lake; (Wakolosai 1:13)
3. Basi kwa kuwa tunapokea ufalme usioweza___________, na mwe na neema, ambayo kwa hiyo___________Mungu ibada ya kumpendeza, pamoja na____________na kicho; (Waebrania 12:28)
4. Lakini walipomwamini______, akizihubiri habari njema za_____wa Mungu, na jina lake Yesu Kristo,_______, wanaume na__________. (Matendo 8:12)
5. na kutufanya kuwa______, na makuhani kwa Mungu, naye ni Baba yake; utukufu na _______una Yeye hata milele na milele. Amina. (Ufunuo 1:6)
6. Mimi Yohana, _____yenu na mwenye kushiriki pamoja nanyi katika mateso na ufalme na subira ya___________, nalikuwa katika kisiwa kiitwacho_____, kwa ajili ya Neno la Mungu, na ushuhuda wa Yesu. (Ufunuo 1:9)

**Majibu:**

1. Watu, mauti, ufalme
2. Kutuingiza, Mwana
3. Kutetemeshwa, tumtolee, unyenyekevu
4. Filipo, ufalme, wakabatizwa, wanawake
5. Ufalme, ukuu
6. Ndugu, Yesu Kristo, Patmo

# Kristo ni Mwokozi wa Mwili

**Sunny David**

Biblia katika Waefeso 5:23 inafundisha kwamba Kristo ni Mwokozi wa mwili Kristo. Sasa mwili ni nini? Mwili ni kanisa. Akizungumza kuhusu Mungu, mtume Paulo alisema, ***"akavitia vitu vyote chini ya miguu yake, akamweka awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa; ambalo ndilo mwili wake, ukamilifu wake anayekamilika kwa vyote katika vyote."*** (Waefeso 1:22-23). Tena, akizungumza kuhusu Kristo, mtume alisema, ***"Naye ndiye kichwa cha mwili, yaani, cha kanisa; naye ni mwanzo, ni mzaliwa wa kwanza katika wafu, ili kwamba awe mtangulizi katika yote."*** (Wakolosai 1:18). Katika mstari wa 24 wa sura hiyo, mtume alisema tena, ***"Sasa nayafurahia mateso niliyo nayo kwa ajili yenu; tena nayatimiliza katika mwili wangu yale yaliyopungua ya mateso ya Kristo, kwa ajili ya mwili wake, yaani, kanisa lake;"***

Kwa hiyo, mwili ambao Kristo ni Mwokozi wake ni kanisa. Katika kusema Kristo ni Mwokozi wa mwili, mtume alikuwa akisema kwamba Kristo ni Mwokozi wa kanisa. Sasa swali ni, **"Kanisa gani?"** Yapo mamia na labda maelfu ya makanisa duniani leo hii, yenye tofauti ya majina, na yanayofuata mifumo mbalimbali ya kuabudu na kufundisha mafundisho tofauti. Katika karne ya kwanza mtume alipoandika maneno haya, palikuwa na kanisa moja tu lile ambalo Kristo aliahidi kulijenga. Alikuwa amesema kuwa litakuwa, ***"Kanisa langu"*** (Mathayo 16:18). Biblia inasema kwamba Yesu analiongeza kanisa kila siku kwa (Matendo 2:47) wale wanaookolewa kwa kuamini na kutii amri yake (Mk 16:16; Mdo 2:38).

Ni dhahiri, anawaongeza wanaookolewa kwenye kanisa lake na sio kwenye makanisa mengi tofauti. Je! Analijua kanisa Lake? Kanisa lake linavaa jina lake (1 Wakorintho 12:27; Warumi 16:16), na viungo vya mwili wake wa kiroho, kanisa, wanaitwa kwa jina

lake—Wakristo (Matendo 11:26). Wanamwabudu Mungu katika roho na kweli ( Yoh. 4:24 ), na wanajitahidi kubaki katika fundisho la Kristo katika kila jambo (2 Yohana 9). Mtume, katika 1 Wakorintho 12:13, pia alifundisha, ***"Kwa maana katika Roho mmoja sisi sote tulibatizwa kuwa mwili mmoja, kwamba tu Wayahudi, au kwamba tu Wayunani; ikiwa tu watumwa au ikiwa tu huru; nasi sote tulinyweshwa Roho mmoja."*** Karne nyingi kabla ya Mkatoliki yeyote au Madhehebu ya Kiprotestanti kuwepo, kanisa lilikuwepo, watu wote waliookolewa kwa uongozi wa Roho wa Mungu, walibatizwa katika mwili mmoja, yaani, ndani ya kanisa moja. Kwa kuwa Kristo anawaongeza watu wote wanaookolewa duniani katika kanisa lake, kwa hiyo kanisa ni mwili wa waliookolewa duniani.

Kanisa ambalo Kristo alilianzisha, ni kama Safina ya Nuhu. Nuhu na familia yake waliamriwa na Mungu kuingia ndani ya Safina ili waokolewe na gharika hiyo. Mungu alikuwa anaenda kuangamiza viumbe vyote vilivyo hai duniani, isipokuwa vile vilivyomo ndani ya Safina ambayo ilijengwa kulingana na maelezo ambayo Mungu alimpa Nuhu (Mwanzo 6-7). Safina haikuwa mwokozi, bali wale tu walioingia ndani ya Safina ndio waliokolewa kupitia maji. Baadaye, mtume Petro, akiwakumbusha Wakristo kuhusu Safina ya Nuhu na nafsi nane zilizookolewa ndani yake pindi maangamizi ya wale waliokuwa nje ya Safina yalipotokea, aliandika: ***" watu wasiotii hapo zamani, uvumilivu wa Mungu ulipokuwa ukingoja, siku za Nuhu, safina ilipokuwa ikitengenezwa; ambamo ndani yake wachache, yaani, watu wanane, waliokoka kwa maji. Mfano wa mambo hayo ni ubatizo, unaowaokoa ninyi pia siku hizi; (siyo kuwekea mbali uchafu wa mwili, bali jibu la dhamiri safi mbele za Mungu), kwa kufufuka kwake Yesu Kristo."*** (1 Petro 3:20-21).

Jambo ambalo mtume alilokuwa akilisema ni kwamba wale waliokuwa ndani ya Safina waliokolewa kwa njia ya maji. Ni maji ya gharika ambayo yalimtengana Nuhu na kizazi kisichotii cha wakati wake, na ni maji ya ubatizo ndiyo yanayowatenganisha waliookoka wa siku hizi na wasiotii. Kristo aliamuru, ***"Aaminiye na kubatizwa***

***ataokoka; asiyeamini atahukumiwa"*** (Marko 16:16). Maji yaliyokuwa ndiyo njia ya maangamizi kwa wengine ndiyo hayohayo ambayo yalikuwa njia ya Nuhu aliyoitumia na watu wa nyumbani mwake wakakombolewa kutoka katika ulimwengu wa zamani wa uovu. Huo ni mfano kati ya ukombozi mbili ule ambao Nuhu alikombolewa kwa maji na ule ambao waamini waliookoka kwa njia ya ubatizo wa maji. Ubatizo, mtume alisema, ni mfano wa maji ambayo Nuhu aliokolewa ndani ya Safina.

Katika hali zote mbili maji yanahusika. Katika ubatizo kuna picha au taswira ya kifo cha Kristo, kuzikwa na kufufuka kwake (Warumi 6:3-4). Mtu anayebatizwa anatambua kwamba ubatizo unaokoa, kwa maana hiyo hali inayotakiwa na Mwokozi na kwamba, kwa kweli, wokovu huja kupitia ufufuo wa Kristo. Ufanisi wa ubatizo katika wokovu haitegemei kazi iliyofanywa bali juu ya ufufuo wa Yesu Kristo, ambayo inafananishwa na kifo cha Kristo. Ndio msingi wa imani na tumaini letu.

Ni maji ya gharika ambayo yaliosha uchafu wa kizazi hicho kiovu, na ni maji ya ubatizo ndiyo ambayo huosha na kuondoa dhambi (Ufunuo 1:5). Yaliyopita yaliathiri mwili na si dhamiri, wakati yajayo yanaathiri dhamiri si mwili. Hata



hivyo, mtu anawezaje kuwa na dhamiri njema ikiwa yeye anakataa kubatizwa kwa ondoleo la dhambi au kuoshwa dhambi, kama Biblia inavyofundisha ( Matendo 2:38; 22:16 )?

## Mungu

# Je! Uliuliza Swali Lolote Zuri Leo?

Russ Vickers

Isidor Isaac Rabi, mmoja wa wanafizikia bora wa Marekani, akawa mwanasayansi kwa sababu moja kuu. Alisema, "Nisingeweza kujizuia." Aliletwa katika nchi hiyo kama mtoto mchanga, hajawahi kusahau swali la kila siku la mama yake kila aliporudi nyumbani kutoka shuleni huko mnara wa Manhattan Upande wa Mashariki: "Je, uliuliza maswali yoyote mazuri leo?"

Maswali mengine ni mazuri kuuliza, lakini mengine si mazuri na yanaweza kuwa ya wakati usiofaa. Chukua kwa mfano, simulizi ya Yesu wakati akimponya mtu aliyezaliwa kipofu katika Yohana 9:1-12. Tunasoma katika mistari 1-2, ***"Hata alipokuwa akipita alimwona mtu, kipofu tangu kuzaliwa. Wanafunzi wake wakamwuliza wakisema, Rabi, ni yupi aliyetenda dhambi, mtu huyu au wazazi wake, hata azaliwe kipofu?"*** Maswali mengine yanaonekana katika kitabu hiki, pia. Katika mstari wa 8 tunasoma, ***"Basi jirani zake, na wale waliomwona zamani kuwa ni mwombaji, wakasema, Je! Huyu siye yule aliyekuwa akiketi na kuomba?"*** Katika mstari wa 10, ***"Basi wakamwambia, Macho yako yalifumbuliwaje? "*** Walakini, kati ya maswali haya yote lilikuja moja ambalo linajitokeza mara nyingi, na ni hilo moja ambalo watu wengi huuliza kuhusu Mwokozi leo: ***"Wakamwambia, Yuko wapi huyo?"*** (Mst. 12).

Inashangaza jinsi watu walivyokazia fikira zao katika maswali hayo. Hata hivyo, swali moja katika mstari wa 12 ni moja la kufaa kuzingatiwa. Jibu zuri ingekuwa kauli ambayo Paulo aliisema katika Matendo 17:27, ambapo Luka aliandika, ***"ili wamtafute Mungu, ingawa ni kwa kupapasa-papasa, wakamwone, ijapokuwa hawi mbali na kila mmoja wetu."***

Inahitajika kwa wanadamu kumtafuta Bwana, ingawa hayuko mbali kutoka kwetu. Je, Bwana yu karibu nasi kivipi? Yeye ni sehemu muhimu ya maisha yetu. Yeye hutupatia uhai, uwezo wa kutembea, kufikiri na kuwepo kwetu. Sulemani alisema kazi yote ya mwanadamu ni kumcha Mungu na kushika amri zake (Mhubiri 12:13 ). Yeye yuko karibu nasi kila dakika ya kila siku. Anajua yote kuhusu sisi.

Yuko wapi? Yuko karibu kuliko unavyoweza kufikiria!

**MUNGU**

# Maneno Saba ya Mwisho

**Mark N. Posey**

Yesu Kristo alizungumza maneno saba ya mwisho wakati wa saa zake za mwisho msalabani. Wakristo wanathamini misemo hii kwa sababu inatoa ufahamu katika kina cha mateso yake ili kukamilisha ukombozi. Maneno saba ya mwisho ya Yesu yanaonyeshwa hapa kwa mpangilio wa matukio.

1. **Neno la Msamaha:** *"Baba uwasamehe"* (Luka 23:34). Yesu aliomba kwa ajili ya wengi ambao walimweka msalabani. Kwa kufanya hivyo, aliitimiza Mathayo 5:44. Sisi pia tulijumuishwa (Warumi 5:8; Yohana 3:16). Yesu alitimiliza unabii, ***"Na kuwaombea wakosaji"*** (Isaya 53:12).
2. **Neno la Wokovu**: *"Leo hivi utakuwa pamoja nami peponi"* (Luka 23:43). Uongofu huu unaweza kuonekana kuwa si wa haki, hata hivyo, Yesu ni mkweli katika neno lake la Neema. Paradiso *(paradeisos)* linawakilisha Mbinguni, uwepo wa Mungu (2 Wakorintho 12:4).
3. **Neno la Upendo:** *"Mama, tazama, mwanao"* (Yohana 19:26-27). Yesu alionesha thamani na umuhimu wa kutokuwa mbinafsi. Hata wakati wa mwisho bado aliwafikiria wengine. Wakristo hawajitazami wenyewe, wanakuwa kama Kristo na kutafakari ya Mbinguni (Wakolosai 3:1-4).
4. **Neno la Kukata tamaa:** *"Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?"* (Mathayo 27:46). Maneno haya ya kujirudia yanaonesha maumivu makubwa aliyokuwa akiyapitia Yesu msalabani na kutimiza unabii katika Zaburi 22. Maneno haya pia yanaonesha uhusiano wa karibu na Mungu kwa sababu kwa sababu alikuwa akiambiwa Yeye.
5. **Neno la Mateso ya Mwili:** *"Nina kiu"* (Yoha 19:28). Yesu alikataa kinywaji cha kutuliza maumivu (Marko 15:23) akichagua kupitia

vikamilifu maumivu na mateso ya kusulibiwa. Sasa, akipokea sponchi ya Hisopo iliyonyanyuliwa juu ambayo ilikuwa na mvinyo laini (siki) kwa ajili ya kukausha midomo na koo ili aweze kulia kwa sauti kuu.

6. **Neno la Ushindi:** *"Imekwisha"* (Yoha 19:30). Nene *tetelestai*, (***"imekwisha"***) lilikuwa likiandikwa kwenye nyaraka za kibiashara au risiti katika nyakati za Agano Jipya kuanshiria kwamba deni limelipwa lote. Yesu alilipa deni letu lote msalabani. Yesu alikuja duniani kumpatanisha mwanadamu na Mungu; alifanya hivyo msalabani.
7. **Neno la Kujitolea:** *"Baba, mikononi mwako naiweka roho yangu"* (Luka 23:46). Pindi kazi yake ilipokwisha, Yesu alikabidhi Roho yake kwa Baba. Alifanya hivi kwa wakati na namna alivyotaka. Yesu hakuwa mhanga wa kuhurumiwa, bali mshindi wa kutamaniwa na kupendwa. Basi tusisahahu kwamba Yesu alikufa kwa ajili yako na mimi.

# Je! Ulijua?

Rebecca Rushmore

Katika 1 Wathesalonike Paulo anawaandikia wasomaji wake, "***Furahini siku zote; ombeni bila kukoma shukuruni kwa kila jambo, maana hayo ni mapenzi ya Mungu kwenu katika Kristo Yesu***" (5:16-18). Ikijieleza katika muktadha wa kufurahi - kujua kwamba Mungu ni mtawala, kwamba Kristo ni mshindi na kwamba, kwa njia ya Kristo tunashiriki katika ushindi huo (Ebr. 12:2; Yak. 1:2)-Paulo anatuagiza tuombe, bila kukoma, na kama sehemu ya hili, tutoe shukrani zetu kwa Mungu kwa yote ambayo ametufanyia. Vitabu vya Injili vimeshiba marejeleo ya Kristo akitafuta faragha ili kumfikiria Baba katika maombi. Maisha yetu yanapojawa na Uradhi na Amani, tunapaswa kusali kwa Mungu, tukimshukuru kwa baraka zake zote. Tunapokuwa tumejawa na majaribu na shida-zinazoletwa na mapambano, mateso na maafa – ni kiasi gani zaidi tunapaswa kumgeukia Mungu katika maombi? Omba bila kukoma. Unapokabiliana na chaguzi kubwa na maamuzi ya maisha, mkaribie Mungu kwa njia ya maombi na umwonyeshe kwa moyo wako wote kibali cha utawala wake maishani mwako kwa kile anachokiona kuwa ni bora zaidi kwako.

## Tarajia

Baada ya kuomba maombi kama hayo, uwe na matarajio (uamini) kuwa Mungu atakuwa mwaminifu na atatendalililojema

kwako. Kwa mtazamo, hapa, ninaamini, inampa zaidi kile kibali cha kutawala kwa ubora. Tena na tena, katika huduma yake Yesu duniani, aliwauliza wale waliomwendea kuhusu imani yao. Katika Injili ya Marko, baada ya kugeuka sura, Kristo alijiliwa na mtu ambaye mtoto wake alikuwa amepagawa na pepo, ambaye alimwomba amtoe, wanafunzi wakiwa hawajafanikiwa katika jitihada zao. "***Yesu akamwambia, Ukiweza! Yote yawezekana kwake aaminiye. Mara babaye yule kijana akapaza sauti, akasema, Naamini, nisaidie kutokuamini kwangu***." (Mk. 9:23-24). Ninaamini kwamba maelezo hayo-na mengine kama hayo ambayo yanasisitiza imani ya mwombaji – yanatufikishia ukweli wa kiroho unaoturekebisha, ambao mara nyingi hupuuzwa: Mungu ametupa uhuru wa kuchagua na anaiheshimu zawadi hiyo, licha ya maamuzi mabaya tunayoyafanya. Walakini, kama – kupitia imani – tunampa kibali cha kutawala maishani mwetu, ili atuelekeze kwa wema huo mkuu kupitia wazo lake la kujua yote, ninaamini kwamba atatawala. Mpe kibali hicho. Mwamini kusudi afungue milango ya fursa – au la aifunge. Hatendi daimakama tunavyotarajia na wakati tunaotarajia, lakini **hutenda**. Inatupasa tuwena subira (Zab. 27:14; 46:10). Kwa kuongezea, tunapaswa kuzingatia kwamba hata "Hapana" linaweza kuwa jawabu la maombi kama vile ilivyo "ndiyo."

## Tafakari

Katika Mwanzo 24:63, tunaambiwa kwamba kabla ya kuwasili kwa mke wake mtarajiwa, Rebeka, Isaka alitoka kwenda kutafakari kondeni wakati wa jioni. HiviIsaka alikuwa anatafakari juu ya nini? Je, kifo kilichotokea karibu cha mama yake Sara? Umri wa uzee wa baba yake Ibrahimu? Au je, maisha yake ya baadaye, ikiwa ni pamoja na matarajio ya mwenzi wake? Maandiko hayatuambii, na

hivyo hatujui. Kiukweli, hata hivyo, tafakuri zake zilihusisha kwa namnafulani zilikuwa juu ya maswala yake mwenyewe kuhusu maisha, kazi za Mungu wa baba yake, Ibrahimu, na jukumu lake mwenyewe katika mpango wa Mungu. Hii inaonekana kuhusishwana muktadha wa simulizi. Lakini, baada ya kushuhudia matukio yaliyoelezewa katika Mwanzo 22 na ushiriki wa jukumu kuu katika matukio hayo, asingeweza kuwa hajui maswala haya. Sisi pia, tutafanya vyema kukumbuka, kuwaza, kutafakari juu ya chaguzi zetu katika maisha, tukipima na kufikiria faida na hasara za chaguzi zinazotukabili; tukiuliza, si tu kusema, "***Ni kitu gani ninahisi kuwa bora kwangu na kwa ajili yangu?***" Lakin pia tuseme, "Mungu anataka mimi nifanye nini?" (Mt. 6:33).

## Tenda

Baada ya kuomba, tukiwa tumeweka tumaini letu kwa Mungu ili atuongoze na kutafakari juu ya chaguzi zinazotukabili, tunapaswa kutenda, daima tukijitahidi kuwa wasikivu kwa kutawaliwa na Mungu, tulimualika Mungu awe sehemu ya jithada zetu na kumpa sifa na kututangulia katika maamuzi ya maisha (Yak. 4:13-15). Tunapotenda tunapaswa kukumbuka agizo la Paulo kwa Wakolosai, "***Na kila mfanyalo, kwa neno au kwa tendo, fanyeni yote katika jina la Bwana Yesu, mkimshukuru Mungu Baba kwa yeye***" (Kol. 3:17).

## Kumbuka

Katika Biblia yote, Agano la Kale na Agano Jipya, watu wa Mungu wanaitwa kukumbuka. Kutangatanga kwa Wayahudi wakati wa kipindi cha Kutokailiwekwa alama na Mungu akiwaamuru wajenge madhabahu ili kukumbuka yale aliyowatendea. Katika

chumba cha juu, Kristo alianzisha Meza ya Bwana ili wafuasi wake wote wakumbuke yale yaliyokuwa yakitendeka na Yeye, kwa uwezo wa Mungu. Kwa njia hizi kuu, mfano wa kukumbuka unatolewa kwetu kwa njia ya imani inayojenga.

Tunapotazama nyuma juu ya maisha yetu, tunaweza kuona kwa uwazi zaidi mwongozo na majaliwa ya Mungu. Tukiwa katikati ya matukio ya maisha, tukiwa na mahangaiko ya kimwili, utata wa mahusiano ya kibinadamu na vikengeusha fikra ambavyo ulimwengu huvitoa, mara nyingi ni vigumu kumwona Mungu akitenda katika maisha yetu. Hata hivyo katika mtazamo wa nyuma, kupitia lenzi ya imani, tunaweza kuona wazi zaidi jinsi alivyotembea maishani mwetu, akitoa fursa, akipunguza wasiwasi katika mahusiano, akipanua nyakati muhimu za amani ya kiakili na kihisia, na uwazi, na hivyo kusaidia azimio na hatua, kufunga milango ambayo hapo awali ilionekana kuleta maendeleo, kuzuia makosa, kuleta watu muhimu katika maisha yetu na - kwa njia nyingine nyingi - kufanya njia za maisha kuwa nyoofu na laini zaidi. Mtazamo huu unahitaji imani, lakini pia husaidia na kujenga imani yetu. Basi tujitahidi kujenga imani yetu. Kwa kufanya hivyo, tufanye upya shauku na uwajibikaji wetu na kuishi jinsi anavyotutaka tuishi.

Kama wana wa Mungu, tunajifunza kuwa kama yeye. Namna anavyoshughulika na sisi, pia ndio inakuwa namna yetu ya kutendeana.

**Neema –** Kwa wale wanaostahili au kutostahili upendeleo wetu.

**Huruma –** Kwa wale wanaoteseka.

**Msamaha –** Kwa wale wanaotubu na kuomba.

**Upatanisho –** Pamoja na wale waliosamehewa.

# Vilivyokithiri Huzaa Vilivyokithiri

## Raymond Elliot

Nakumbuka vizuri maneno haya yaliyosemwa na mwalimu wangu mwenye busara na maarifa nilipokuwa chuoni. Ndugu Rex A Turner, Sr. alikuwa na "Misemo" mingi, lakini huu ndio ninaotaka kuusisitiza kwa sasa. Nimeishi muda wa kutosha (miaka 83) kujua kiukweli na kwa uzoefu kwamba huu ni ukweli katika jamii yetu ya leo. Pia alisema kwamba mtu anahitaji "Gurudumu lenye Uwiano" ambalo tunalihitaji sana leo. Sisi ni watu wenye msimamomkali. Hili lina ushahidisana katika ulimwengu wa kisiasa. Inaonekana, hakuna uwanjawakatikati kwa baadhi ya viongozi wetu waliochaguliwa na katika jamii kwa ujumla. Kwa kweli inahuzunisha kushuhudia ubaguzi na chuki vinadhihirika katika nchi yetu. Unaweza kuiona halikama hiyo kwa watu wenye historia ya makabila na maadili tofauti. Unapotazama habari kwenye televisheni au unposoma magazeti, unaweza kuona na kuhakikishiwa kwamba vitendo vya hali iliyokithiri kama hivyo vya mtu mmoja mmoja na makundi ya watu vinaripotiwa.

Ninakumbushwa habari ya ufunguzi katika kitabu kinachoitwa, ***Simulizi ya miji miwili*** (1857), kilichoandikwa na Charles Dickens.

> Zilikuwa nyakati bora zaidi, zilikuwa nyakati mbaya zaidi, zilikuwa zama za hekima, zilikuwa zama za upumbavu, kilikuwa kipindi cha imani, kilikuwa kipindi cha kutoamini, yalikuwa majira ya nuru, yalikuwa majira ya giza, lilikuwa joto la

> matumaini, yalikuwa majira ya baridi ya kukatisha tamaa, tulikuwa na kila kitu, hatukuwa na kitu chochote, sote tulikuwa tunaenda mbinguni moja kwa moja, sote tulikuwa tukielekea njia nyingine-kwa kifupi, kipindi kilichofika mbali sana kama ilivyo kwa kipindi cha sasa, kiasi kwamba baadhi ya mamlaka zake zenye kelele zaidi zilisisitiza juu ya kupokelewa kwake, kwa mema na kwa maovu, kwa kiwango cha juu zaidi cha ulinganifu tu.

Kwa ufupi, maelezo ya jamii ambayo mwandishi aliishi yanajifafanua kwa njia nyingi, hali na matendo ya sasa yaliyokithiri ya wakati wetu.

Kama wakristo, tunapaswa kufuata mafundisho ya Yesu Kristo aliyesema, "***Heri wapatanishi; Maana hao wataitwa wana wa Mungu***." (Mt. 5:9). Mtume Paulo anaandika katika Warumi 12:17-18, "***Msimlipe mtu ovu kwa ovu. Angalieni yaliyo mema machoni pa watu wote. Kama yamkini, kwa upande wenu, mkae katika amani na watu wote***." Katika Waebrania 12:14, tunasoma, "***Tafuteni kwa bidii kuwa na amani na watu wote, na huo utakatifu, ambao hapana mtu atakayemwona Bwana asipokuwa nao***." Hatupaswi tu kuwa watoto wa Mungu ambao wana, "***amani ya Mungu, ipitayo akili zote***" (Flp. 4:7), lakini lazima tuwe "***wapatanishi***" katika kanisa na katika jamii. Hiyo, rafiki zangu, ni changamoto kubwa kwa wote wanaomfuata "***Mfalme wa Aman***i" (Isa 9:6). Ifuatayo inapaswa kuwa sala ya Wakristo wote.

> Bwana, nifanye chombo cha amani yako. Palipo na chuki, nipande upendo. Palipo na maumivu, msamaha. Palipo nashaka, imani. Palipo na kukata tamaa, matumaini. Palipo na giza, nuru. Palipo na huzuni, furaha. Ee Bwana Mungu, nijalie nisitafute sana kufarijiwa bali kufariji, kueleweka kama kuelewa, kupendwa kama kupenda (Francis wa Assisi).

# Maoni ya Haraka katika Aya Muhimu

## (Wafilipi 4:12-18)

***12*** Najua kudhiliwa, tena najua
kufanikiwa; katika hali yo yote, na
katika mambo yo yote,
nimefundishwa kushiba na kuona
njaa, kuwa na vingi na
kupungukiwa. ***13*** Nayaweza
mambo yote katika yeye anitiaye
nguvu. ***14*** Lakini mlifanya vema,
mliposhiriki nami katika dhiki
yangu. ***15*** Nanyi pia, ninyi
wenyewe mnajua, enyi Wafilipi, ya
kuwa katika mwanzo wa Injili,
nilipotoka Makedonia, hakuna
kanisa lingine lililoshirikiana nami
katika habari hii ya kutoa na
kupokea, ila ninyi peke yenu.
***16*** Kwa kuwa hata huko
Thesalonike mliniletea msaada
kwa mahitaji yangu, wala si mara
moja. ***17*** Si kwamba nakitamani
kile kipawa, bali nayatamani
mazao yanayozidi kuwa mengi,
katika hesabu yenu. ***18*** Lakini
ninavyo vitu vyote na kuzidi, tena
nimejaa tele; nimepokea kwa
mkono wa Epafrodito vitu vile
vilivyotoka kwenu, harufu ya
manukato, sadaka yenye kibali,
impendezayo Mungu.

Maneno haya yanapaswa kuwa ndiyo tabia ya maisha ya kila Mkristo. Tunajikuta tupo katika changamoto nyingi, lakini ikiwa matatizo yetu ni matokeo ya kujitoa kwetu thabiti kwa Kristo, basi tunapaswa kuwa na tabia ya kumwamini Mungu kwamba atatutazama katika kila changamoto.

Katika kujibu uhitaji wa kifedha wa Paulo uliotokana na kufungwa gerezani, alithibitisha kwamba mtenda kazi katika ufalme anaweza kupokea msaada wa kifeha kutoka kwa makusanyiko mengi. Ni wazi kwamba ndugu wa Filipi walitambua uhitaji wa Paulo na wakamtumia fedha zaidi ya mara moja.

Pia tunasoma katika 1 Kor. 16:1-2 kwamba Paulo alikusanya fedha kutoka kwa makusanyiko mbalimbali na kuwapelekea ndugu waliokuwa wakiteseka huko Yerusalemu.

Fedha za kanisa na fedha za Mkristo mmoja mmoja ni mali ya Mungu. Badala ya kutumia kwa matumizi yasiyo ya kimaandiko, tunapaswa kuzitumia iwe kwa kukusanya au fungu moja moja kwa ajili ya kueneza Injili.

# Kumbuka Wewe ni wa NANI

Curtis D. Burton

Mungu ni lengo kuu la maisha yangu. Simaanishi kwamba Mimi ni mkristo niliyekamilika au kwamba mimi ni mfano mzuri wa mkristo wakati fulani, lakini kila siku ninapoamka ninachagua kumfuata Mungu kwa kadri ya uwezo wangu.

Kadiri ninavyozeeka, nilivyosoma na nilivyochunguza nimekuwa nikifadhaishwa zaidi na shambulio dhidi ya Mungu ambalo nimeshihudia (kuwepo kwake), Biblia na dini kwa ujumla. Nilipokuwa kijana katika miaka ya 60/70, dini bado ilionekana kuwa suluhisho la matatizo mengi ya ulimwengu. Lakini muda ulivyosonga mbele kufikia siku za sasa, dini inaonekana kama shida badala ya suluhisho.

Wakristo wanadhihakiwa waziwazi, wanafanyiwa mzahana kudharauliwa. Tunaonekana kuwa wahukumu, wabinafsi na wenye chuki.

Marekani imekuwa tajiri na "imeelimika," wengi, *hataviongozi wa kanisa* wamefikia hatua ya kusema kwamba Biblia si neno la Mungu, si halisi, na si la kweli. Wanadiriki kusema kwamba, "...ni mkusanyiko tu wa simulizi nzuri zilizofikiriwa na wazee wa zamani ili kushikilia mamlaka yao na kuwanyanyasa wanawake na maskini.

Unaweza kufikiri hizo ni kauli zilizopindukia, lakini miaka michache iliyopita, mzee wa zamani katika "kanisa la Kristo" hapa Texas aliniambia, "hakika wewe ni wa kisasa zaidi kuliko kuamini kwamba Nuhu alikusanya Wanyama wote ndani ya safina na kuishi nao humo kwa zaidi ya mwaka mmoja! Bwana huyo huyo alisema kwamba hakuna ubaya wowote kuwepo na tabia ya ushoga kwa sababu "Mungu aliwaumba hivyo." Maneno yake ya kuondokea

yalikuwa, “Na hiyo hadithi ya kipuuzi ya samaki kuhusiana na Yona. Una elimu ya chuo, jamani, hakika unatambua kwamba hadithi hizo zilikuwa ni vielelezo tu vya hoja zilizokuwa zikitolewa katika maandishi...si matukio halisi.”

Taasisi za kijografia za Taifa, ABC, NBC, CBS, chaneli ya historia na wanatheolojia wengi hata katika vyuo vikuu vyetu vya kidini wanadhihaki waziwazi wazo la kwamba Biblia imevuviwa au kitu chochote zaidi ya mkusanyiko wa "hadithi."

Halafu kuna swala zima hili lamabadiliko ya viumbe ambalo limeota mizizi. "Hakuna MTU ALIYESOMA ambaye kwa umakini anaweza kubisha kwamba uhai ulikuja na kusitawi si kwa njia yoyote ZAIDI YA mabadiliko ya viumbe...", ndivyo alivyosema mtu msomi kama Stephen Hawking. Yote yananiweka akilini mwa Warumi 1:28-33:

> "***Na kama walivyokataa kuwa na Mungu katika fahamu zao, Mungu aliwaacha wafuate akili zao zisizofaa, wayafanye yasiyowapasa. Wamejawa na udhalimu wa kila namna, uovu na tamaa na ubaya; wamejawa na husuda, na uuaji, na fitina, na hadaa; watu wa nia mbaya, wenye kusengenya, wenye kusingizia, wenye kumchukia Mungu, wenye jeuri, wenye kutakabari, wenye majivuno, wenye kutunga mabaya, wasiowatii wazazi wao, wasio na ufahamu, wenye kuvunja maagano, wasiopenda jamaa zao, wasio na rehema; ambao wakijua sana hukumu ya haki ya Mungu, ya kwamba wayatendao hayo wamestahili mauti, wanatenda hayo, wala si hivyo tu, bali wanakubaliana nao wayatendao.***"

Je, uko kama ulimwengu ambao kwao unaishi? Hakika inaumiza ile hali ambayo mimi nashughulika nayo kila siku. Wakati fulani hilo linanihuzunisha.Naona majeshi ya maovu yako juu

yangu,na wakati mwingine hata mimi najiona kama sehemu yake ninaposhindwa kuishi inipasavyo kama mfuasi [wa Kristo]. Mambo yanatuzidi mno, na shetani anaonekana kushinda katika nyanja nyingi sana. Ni katika nyakati hizo hasa tunapoona nguvu za shetani na ulimwengu ulioanguka juu yetu kwamba tunahitaji kukumbuka sisi NI WA NANI.1 Petro 2:9-12 tunaambiwa:

> "***Bali ninyi ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa MILIKI ya MUNGU, mpate kuzitangaza fadhili zake yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru yake ya ajabu; ninyi mliokuwa kwanza si taifa, bali sasa ni taifa la Mungu; mliokuwa hamkupata rehema, bali sasa mmepata rehema. Wapenzi, nawasihi kama wapitaji na wasafiri, ziepukeni tamaa za mwili zipiganazo na roho. Mwe na mwenendo mzuri kati ya Mataifa, ili, iwapo huwasingizia kuwa watenda mabaya, wayatazamapo matendo yenu mazuri, wamtukuze Mungu siku ya kujiliwa***."

Wito huo huo unatolewa kwetu leo. Tunaweza kwenda huku na huku tukiwa na mtazamo mbaya na wenye kupinga mani yetu, AU tunaweza kuwa watu wenye furaha, tukiishi katika njia INAYOMPA UTUKUFU MUNGU kuliletea jina lake takatifu. Hiyo ina maana kwamba tunapaswa kuzungumza juu ya kile ambacho kitabu chake kinasema, si kwa kugombana, wala kwa chuki, bali kwa upendo tukiuambia ulimwengu unaoumwa tena unaelekea kufa, kwamba kuna MUNGU MBINGUNI AMBAYE ALIKUPENDA SANA HATA AKAMTOA MWANAWE WA PEKEE ILI UPATE UZIMA WA MILELE PAMOJA NAYE.

Kwa hiyo, unapokwenda ulimwengu leo, kumbuka mambo mawili. "**Kumbuka WEWE NI NANI, na kumbuka WEWE NI WA NANI**." Kila kitu kitajipanga chenyewe.

# Mkinipenda

## Andy Robison

Wengi wanasema kuwa wanampenda Yesu. Ni wangapi watakaofanya kweli na watakaoamuliwa na Hakimu Mwenye Haki katika Siku ya Mwisho (2 Timotheo 4:8). Wale ***"waliopenda kufunuliwa Kwake"*** watakuwa ni wale ambao wametayarishwa kulingana na masharti ya Yesu. Maneno hayo yanafichuliwa; sio siri. Maneno ya Kristo yaliyofunuliwa yatakuwa kipimo cha hukumu katika Siku ya Mwisho (Yohana 12:48). Maneno haya yanajumuisha yale yaliyofunuliwa kwa mitume na manabii kwa Roho waliyepewa baada ya Kupaa kwa Yesu (Yohana 16:13; Matendo 2:33; Waefeso 3:5; Waebrania 1:1-3). Hakuna kubahatisha katika kile kinachohitajika kwetu.

Kwa kweli, mtu anaweza kupendelea kukisia (nazungumza kwa utani). Watu wengi wanaonekana kupendelea. Kuna tabia katika ulimwengu wa Jumuiya ya Wakristo ambayo husisitiza upendo, lakini upendo huo unafafanuliwa upya kulingana na ulimwengu wa kisasa. Jamii za kisasa—wengine husema jumuiya za Ukristo—zinasisitiza usawa wa mifumo yote ya imani. Hakuna ukweli katika mtazamo huu wa ulimwengu (isipokuwa, bila shaka, kejeli inayoharibu mafundisho ambayo "ukweli ni kwamba hakuna ukweli"). Upendo kwa mitazamo yote ya ulimwengu unafafanuliwa kama kitu kamili kilichohidhinishwa na kukubalika.

Falsafa hii ya kidunia inaenea katika mawazo ya Mkristo ambaye anatamani msuguano mdogo na ulimwengu. Upendo tu. Usisome juu ya kutokubaliana. Usiwe na lengo la ***"kusema kitu kimoja"*** (1 Wakorintho 1:10). Upendo tu. Mpende Yesu, na wapende watu. Hiyo ndiyo yote unayohitaji. Hili ni fundisho kamili la watu wa dunia ya sasa (Postmodernism).

Hata hivyo, Mwokozi wa ulimwengu alifafanua upendo. ***“Mkinipenda, mtazishika amri zangu”*** (Yohana 14:15). Mawaidha hayo yasingeweza kupita katika upana wake [hekima]. Yamewekwa karibu katika kila ukurasa wa Maandiko. Kwa mifano mifupi, fikiria Yakobo 1:22 . ***“Iweni watendaji wa neno, wala si wasikiaji tu…”*** Fikiria Mathayo 7:21, inayosomeka, ***“Si kila mtu aniambiaye, Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyaye mapenzi. ya Baba yangu aliye mbinguni.”*** Tafakari kuhusu vielelezo vingi vya jinsi ***“imani pasipo matendo imekufa”*** (Yakobo 2:14-26).

Vifungu hivi, na vingine vingi, vinaharibu sana fundisho la “imani pekee,” fundisho la “neema pekee” na fundisho la “upendo pekee”. Mchanganyiko wa Yohana 14:15 na Yohana 12:48 humlazimu anayempenda Mungu kuchimba kwa kina ndani ya Neno daima, kwa uaminifu na kwa bidii ili kuona amri hizo zilivyo. Yule anayempenda Bwana atataka kumpendeza. Mtu hawezi kumpendeza bila kujua amri zake. Mtazamo wa "kufikiri hivyo" hautafanya kazi. Amri zimefunuliwa. Basi, ujuzi huo lazima uzae utii.

Inaonekana kwamba kujifunza katika Neno ni mtihani wa upendo mwenyewe. Je, yule anayedai kuwa mfuasi ana upendo wa kutosha kuweka juhudi za kutafuta mapenzi ya Bwana?

## NGUVU YA UPENDO

Shadrack S. Msambaza

Kiunganishi cha amri zote za Agano la Kale, Bwana alisema ni “UPENDO” (Marko 12:28-31). Katika Agano Jipya vivyo hivyo “UPENDO” unabaki kuwa ndio kiunganishi cha amri zote (Yohana 15:12). Lakini kwa nini? Vizuri, ni kwa sababu ukimpenda Mungu bila shaka utatekeleza amri nyingine kwa hiari pasipo hata kujua kuwa unatekeleza. Kwa jirani vivyo hivyo, kamwe hutaweza kumtendea vibaya mtu unayempenda. Hii ndiyo kanuni!

# SEHEMU YA UPONYAJI

**Randal Matheny**


Katika tovuti ya hivi majuzi ya mtandao wa kijamii, nilianzisha jumuiya ndogo inayoitwa "Njia ya Kristo." Mtu yeyote anaweza kuchapisha hapo, kulingana na sheria za tovuti. Mtu mmoja alichapisha picha ya mambo ya ndani ya jumba kubwa la kidini. Alipaita, "mahali pangu pa uponyaji." Mara moja, nilihisi huruma kwake.

Mahali pa uponyaji wa kweli na wa milele ni katika Yesu Kristo. Katika mwili wa Kristo, ambapo karama za washirika wote zinatumika, roho hutunzwa. Katika familia ya imani, ninapata faraja na nguvu.

Mahali pangu pa uponyaji ni katika ushirika wa Mungu, upendo wa Kristo na nguvu za Roho Mtakatifu. Pahali pangu pa wokovu wa kiroho na kutumika na kuwa na kaka na dada zangu katika Kristo. Eneo la kimwili la kukutania.

Ilitokea tena jana usiku. Kuimba, kuomba na kusoma Maandiko pamoja na marafiki wa Kristo, pamoja na watu kadhaa wa nje waliopendezwa, kulileta burudani katika nafsi yangu. Mojawapo ya mambo bora zaidi kuhusu mahali hapa pa uponyaji ni kwamba inapatikana kila mahali duniani. Hakuna hija zinazohitajika. Badala ya kutembelea mara kwa mara, kila nafsi moja inaweza kukaa katika mahali pa uponyaji pa Mungu.

Sisi sote tunahitaji uponyaji wake. Anatualika mahali pake, katika Kristo. Anamkaribisha kila mtu kama mtoto wake wa thamani. Hapa, wakati bado kuna, mlango ulio wazi. ***"Lakini kwa kutenda kwake ninyi mmekuwa ndani ya Kristo Yesu, aliyefanyika kwetu hekima itokayo kwa Mungu, na haki, na utakatifu, na ukombozi"*** (1 Wakorintho 1:30).



# JE! UNAPIMAJE?

Ndugu zangu, mnifuate mimi, mkawatazame wao waendao kwa kuufuata mfano tuliowapa ninyi. Maana wengi huenenda, ambao nimewaambieni mara nyingi habari zao, na sasa nawaambia hata kwa machozi, kuwa ni adui za msalaba wa Kristo; mwisho wao ni uharibifu, mungu wao ni tumbo, utukufu wao u katika fedheha yao, waniao mambo ya duniani. Kwa maana sisi, wenyeji wetu uko mbinguni; kutoka huko tena tunamtazamia Mwokozi, Bwana Yesu Kristo; atakayeubadili mwili wetu wa unyonge, upate kufanana na mwili wake wa utukufu, kwa uweza ule ambao kwa huo aweza hata kuvitiisha vitu vyote viwe chini yake.

Basi, ndugu zangu, wapendwa wangu, ninaowaonea shauku, furaha yangu, na taji yangu, hivyo simameni imara katika Bwana, wapenzi wangu.

Wafilipi 3:17-21; 4:1

# UANAUME WENYE SUMU

**Victor M. Eskew**

"Uanaume wenye sumu" ni neno ambalo linatupwa sana na vyombo vya habari siku hizi. Neno hilo linamaanisha kuwa uanaume umejaa sumu. Kwa maneno mengine, kuwa mwanaume ni uovu.

[Cha kusikitisha, mara nyingi siku hizi, ni vigumu kuamua kama mtu tunayemwona ni mwanamume au mwanamke. Wanawake huvaa sawasawa na wanaume na mara nyingi hukata wamenyoa nywele zao kama wanaume. Wanaume wanaweza kuwa na nywele ndefu kama wanawake na wakati mwingine mavazi yao ni sawa. Ni nini kimetokea kaika tamaduni zetu na kwa uanaume wa zamani unaoheshimika?]

Ukifanya mambo ambayo tunaambiwa wanaume hawapaswi kufanya, basi umeathirika na sumu. Umepewa sumu. Kuna kitu hakipo sawa kwako.

Katika vifungu viwili vya Maandiko, **Biblia inawahimiza wanaume kuwa wanaume**. Msemo uliotumika ni: ***"fanyeni kiume"*** (1 Samweli 4:9; 1 Wakorintho 16:13). Mungu anataka wanadamu wawe wanaume, watende kama wanaume na kutimiza jukumu alilowapa.


Bila kujali kile "wataalamu" na vyombo vya habari wanavyosema, "Wanaume sio wanawake!" Mwanaume ameumbwa tofauti sana na mwanamke. Kulazimisha wanaume kuwa wa kike ni ufisadi wa jukumu la mwanaume. Wacha wanaume wawe wanaume. Waache wafanye mambo yao ya "kiume".

KUMBUKA: Hii haimaanishi kwamba hawatakiwi kuwaheshimu wanawake. Mwanamume halisi anajua jinsi ya kuwatendea vizuri wanawake wanaomzunguka, mke wake, binti yake, mfanyakazi mwenza na anayekutana naye mitaani.

Rafiki zangu, kwa kukiita tu kitu jina hakufanyi kiwe hivyo. Kwa sababu mtu anafanya kama mwanaume haimaanishi kuwa yeye ni sumu. WANAUME, KUWENI WANAUME! Usiruhusu jamii ikuletee aibu!

# Je! Mungu Anasema Nini Kuhusu Kulea Watoto?

**Darla Rosinski**



Kila jambo katika maisha yetu linapaswa kuanza na kumpenda Mungu kwa moyo wetu wote, roho na uwezo wetu wote! Kuwa wazazi si lazima kuwa jambo la asili, kwa hiyo kuanza na maagizo ya Muumba wetu hutuweka kwenye njia ifaayo.

Mungu hurudia mambo ambayo anataka tuyasikilize kwa makini. Katika Kumbukumbu la Torati 6 na tena katika sura ya 11, Mungu anatuambia tuwafundishe watoto wetu kwa bidii njia yake—**kuzungumza nao unapoketi katika nyumba yako, unapotembea njiani, unapolala na unapoamka.** Hiyo inachukua karibu wakati wote tulionao. Daima kuwafundisha kuhusu Baba yao wa milele! Wanahitaji kujua kwamba Yeye ndiye kiini cha ulimwengu!

Watu wamekuwa wakiamini hekima ya wanadamu wengine kwa muda mrefu sana, hawawezi kamwe kumpiga mtoto, kwa

sehemu wakiogopa kushitakiwa na polisi kwa unyanyasaji wa watoto na kwa sababu wanaamini kile walichoambiwa kuhusu viboko. Mbaya kwa mtoto. Je, Mungu anasema nini kuhusu nidhamu? Mithali 3:11-12 inatuhakikishia kwamba Bwana huwarekebisha wale anaowapenda kama vile baba anavyomrudi mwana ambaye anapendezwa naye. ***“Mwanangu, usidharau kurudiwa na Bwana, wala usichukie kurudiwa na yeye; kwa maana Bwana ampendaye humrudi, kama vile baba mwana ambaye amependezwa naye.”*** Katika sura ya 23:13-14, tunaambiwa, ***“Usimnyime mtoto wako mapigo; Maana ukimpiga kwa fimbo hatakufa. Utampiga kwa fimbo, Na kumwokoa nafsi yake na Kuzimu.”*** Kuna tofauti kubwa ya kumpiga mtoto na kumdhulumu! ***“Fimbo na maonyo hutia hekima, bali mtoto aliyeachiliwa humwaibisha mamaye”*** (Mithali 29:15).

Mara nyingi tunasikia, "Inahitajika kijiji kulea mtoto." Usiamini! Inawahitaji wazazi wanaomcha Mungu kuwafundisha watoto wao kuwa wacha Mungu pia. Je! unataka mtoto wako aishi kama ulimwengu unavyotuambia jinsi tunavyopaswa kuishi? Ulimwengu unatutaka tuamini mambo kama vile: Hakuna Mungu na ni watu dhaifu tu wanaomwamini; tena huwezi kuamini katika Biblia kwa sababu watu wengi wameigusa, haiwezi kuwa sawa; tena ngono kabla ya ndoa ni sawa, tumia tu mpango wa uzazi na ikiwa haifanyi kazi, unaweza kutoa mimba; Haijalishi unachagua kuoana na nani ili mradi tu unaungana na mtu huyo; Familia si Baba, Mama na watoto, ni Baba, Baba na watoto au Mama, Mama na watoto.

Tito 1:2 inatuambia kwamba Mungu hawezi kusema uwongo, na hiyo ina maana kwamba kila ahadi ambayo ametuahidi ni kweli, na tunaweza kuitegemea! Tumeahidiwa ikiwa tutawalea watoto wetu katika njia za Mungu, watakapokuwa wazee, hawataiacha. Ikiwa sisi ni waaminifu hadi tunapokufa, tuna makao Mbinguni kwa umilele (Ufunuo 2:10). Je, hilo si lengo letu kuu, kukaa milele na watoto wetu katika nyumba ambayo Yesu alikufa ili atupatie?

# Maisha ya Kila Siku ya Kikristo

# MABENCHI TUPU

**Charles R. Rose**

***“Msiipende dunia wala mambo yaliyomo katika dunia. Mtu akiipenda dunia, kumpenda Baba hakupo ndani yake”*** (1 Yohana 2:15). Hiyo ni kauli nzito sana kutoka kwa Mungu. Tunapofikiria athari zake, siwezi kujizuia kufikiria jinsi upendo wa vitu vya kidunia unavyokuja kwa urahisi katika akili zetu na hatimaye katika maisha yetu. Tunaporuhusu ulimwengu kuchukua udhibiti, bila kukusudia tunawaongoza wapendwa wetu katika dhambi sawa na sisi wenyewe. Badala ya kuupenda ulimwengu, kama Wakristo, tunapaswa kuwa ***“wafanya kazi pamoja na Mungu”*** (1 Wakorintho 3:9a). Kwa hiyo, lazima tuulize, "Je! upendo wangu kwa roho za marafiki na familia ni wa kina kiasi gani?"

Tunalia machozi ya uchungu wapendwa wetu wanapoaga dunia. Je, uchungu wetu ni zaidi kwa ajili ya kupoteza roho zao au hasara yetu binafsi ya kutokuwa na uwepo wao nasi tena katika ulimwengu huu? Yesu alilia kwa kifo cha rafiki yake Lazaro, lakini kuugua kwake kulikuwa kwa ajili ya roho zilizomzunguka (Yohana 11:33-35). Tamaa yake ilikuwa kwamba waje kuamini na kuwa watiifu kwa Mungu Baba. Paulo alionya, ***“Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu ambayo ilikuwamo pia ndani ya Kristo Yesu”*** (Wafilipi 2:5).

Wakati wa harakati za urejesho huko Scotland, John Knox alialika kikundi cha marafiki nyumbani kwake jioni moja. Aliliacha kundi lile ndani, na wakati fulani baadaye walimkuta kwenye bustani akiwa amepiga magoti huku akiwa katika uchungu mwingi akisema, “Ee Mungu, nipe Scotland kwa ajili ya Kristo au nife!” Ni nini kingenisababisha mimi na wewe kumwomba Mungu atusaidie kuwafikia wapendwa wetu wa karibu na wapendwa zaidi? Tunahitaji kunaswa katika msisimko wa kuleta roho kwa Kristo. Hebu tuwe zaidi ya “washirika wa kanisa” tu. Na tuwe “wafanya kazi

pamoja na Mungu." Hebu na tuombe kwa bidii, "Ee Mungu, tupe jumii hii kwa ajili ya Kristo!"

Katika miaka ya hivi majuzi ninaposimama mbele ya kusanyiko ili kuzungumza, iwe hapa au kwingineko, ninalazimika kutazama viti vingi visivyo na watu. Mara nyingi nimesimama pale nikifikiria juu ya mhubiri ambaye alisema angeweza kumwona Shetani akiwa ameketi kwenye kiti kile kilicho tupu, akimtazama, akicheka na kusema, "Nina huyu leo, mhubiri!" Mawazo haya yalikuwa akilini mwangu huku nikiandika yafuatayo.

Ninapotazama chini kwenye kiti kilicho tupu
Namfikiria, Bwana Mpendwa, kwa nini wachache sana?
Je! Shetani amegeuza kila fikira zao?
Kwa uongo na uovu wake wote uliotendwa?
Najua umesema hayo kupitia lango hilo
Umati wa wanadamu unasubiri.
Na wanaposafiri njia hii ya uzima
-Kutotaka kusikiliza, kumejaa ugomvi -
Umetuacha, wateule wachache,
***Kufanya kazi na kujaza kiti hicho tupu***.

Katika kufikiria wapendwa wetu waliopotea, kila Mkristo ana mzigo wa Agizo Kuu juu yake. Badala ya kupenda ulimwengu na vitu vilivyomo duniani ( 1 Yohana 2:15 ), ni lazima ***"tukisema kweli katika upendo"*** (ili sisi na wapendwa wetu) ***"…tupate kukua katika mambo yote ndani yake yeye aliye Kristo, ambaye kutoka kwake mwili wote ukiungamanishwa na kushikanishwa kwa msaada wa kila kiungo, kwa kadiri ya utendaji kazi ufaao ambao kwa huo kila kiungo hushiriki, huukuza mwili upate kujijenga wenyewe katika upendo"*** (Waefeso 4:15-16).

Tusililetee jina lake takatifu lawama kwa kupuuza nafasi yetu katika makusanyiko ya watakatifu. Na tuwatie moyo na kuwaonya marafiki na familia zetu ili wajaze viti vilivyo tupu tunapomwabudu Mungu mmoja wa kweli na aliye hai.

# Kuponya Huzuni

Sheila Gibson

Uzoefu mwingi wa wanadamu ni wa kawaida kwa kila mtu, lakini ni wa kipekee kwa mtu binafsi: maisha yenyewe, furaha, huzuni na hatimaye kifo. Sisi sote tutakufa, lakini baadhi yetu tunajua huzuni ya kifo, muda mrefu kabla ya sisi wenyewe, kutokana na kupoteza mtu tunayempenda. Au, labda watu wengi tunaowapenda hufa.

Mwaka jana, nilimpoteza mwanangu—mwanangu mrembo, mwenye furaha na wa ajabu. Hatukuona mapambano aliyopitia na hatukuona kuwa yuko hatarini. Hatukufikiria kwamba tungewahi kujua uchungu wa kupoteza kwa kujiua na maswali yanayofuata.

Kwa nini hakuzungumza na sisi? Tumekosa nini? Tungewezaje kumsaidia? Kwa nini hili lilitokea? Kwa nini? Kwa nini? Kwa nini?

Niamini, maswali yanakuja, na hakuna majibu ya kutosha. Yule pekee aliye na majibu hayupo na sisi sasa, na hatuwezi kumfikia-sio katika ulimwengu huu.

Ingekuwa rahisi kujipoteza mwenyewe katika huzuni, kuzama katika mawimbi ya huzuni. Kutokuwepo kwake karibu katika maisha yangu ni kama vile uwepo wake ulivyokuwa. Kama mwanangu kutokuwepo kwake kunatoa taarifa na kutembea karibu nami, na kuchukua nafasi moyoni mwangu ambayo mvulana huyo alikuwa akiijaza.

Kupoteza mtoto, ni uzoefu wa ajabu. Ingawa alikuwa na umri wa miaka 30, lakini hakuna neno kamili la kuelezea hilo. Ni kifo kisichokuwa katika mpangilio. Wazazi wanapaswa kwenda kwanza. Hakuna kitu sahihi kuhusu kuishi zaidi ya mtu uliyemzaa.

Hata hivyo, imeshatokea, na hakuna kinachowezekana kurudisha tukio hilo nyuma. Majivu yake yapo sebuleni kwangu ili kunikumbusha kana kwamba alihitaji hilo.

Kwa hiyo, nimeachwa na kumbukumbu na ujuzi wa jinsi alivyokuwa na tumaini kwa ajili ya baadaye. Nina tumaini la kumwona tena, ili nielewe kwa nini na kujua kwamba yupo katika amani.

Mimi nitakwenda kwake, lakini yeye hatanirudia. ***"Lakini sasa amekufa… Je! Naweza kumrudisha tena? Mimi nitakwenda kwake lakini yeye hatanirudia mimi"*** (2 Samweli 12:23).

Nimeachwa na kielelezo alichokiweka, kujitoa mwenyewe kwa hiari kwa walio wengi.

Alikuwa mkarimu kwa wakosaji.

Alikuwa mcheshi na wa pekee, nuru angavu ambayo ilimleta kila mtu kwake.

Alikuwa ni mzee war oho na mtu wa kutafakari sana, akiongea kirahisi masuala ya roho na moyo.

Alikuwa mchapakazi, mshindani na mwenye bidii.

Alikuwa askari kwa miaka mitano—labda daima moyoni.

Alikuwa mgumu kwa nje lakini mwororo chini ya ganda.

Alikuwa mwanangu na furaha yangu.

Tulijitahidi sana. Walakini, ikiwa mimi ni mwaminifu, nitakubali, katika mengi jinsi alivyokuwa, alikuwa hivyo tangu kuzaliwa. Nuru ilikuwepo kila wakati; tulimlea tu. Siku zote alikuwa mtu wake mwenyewe, kila mara aliandamana kwa mpigo wake. Alifanya uchaguzi wake, hata mwisho.

Kwa kuwa amefariki, kwa kuwa nimeanza maisha haya mapya, mtu ambaye nina shimo katika moyo wangu, nimejifunza mengi sana.

Nimejifunza kuwa upendo ndio jibu. Swali lolote, mwishowe, jibu ni upendo. ***"Mungu ni upendo, naye akaaye katika pendo, hukaa ndani ya Mungu, na Mungu ndani yake"*** (1 Yohana 4:16). Hatimaye, hilo ndilo jibu ninalotaka kuwa nalo, ambalo ninachagua kuwa nalo—kwa uzima, kwa furaha na huzuni.

Kwa hivyo, nampenda Alex. Nitampenda daima. Najua chaguo lake halikuwa la nia ya kuumiza. Llikuwa ni kitendo cha huzuni.

Ingawa siwezi kuponya huzuni aliyokuwa nayo mwishoni mwa maisha yake, ninaweza kuchukua upendo nilio nao kwake na kuwaeleza wengine. Ninaweza kuruhusu uongeze ukarimu kutoka kwa roho yangu kwa wengine kwa heshima yake na kwa sababu ya kumpenda.

Kwa hiyo, mimi hutoa damu, kama alivyofanya, na kuwatia moyo wengine kufanya hivyo.

Nakumbuka furaha ya maisha yake na kusherehekea hilo. Inanitia moyo kupata furaha pale ninapoweza. Hatujui kamwe siku italeta nini, lakini tumeitwa kuwa chumvi na mwanga. ***"Ninyi ni chumvi ya dunia; lakini chumvi ikiwa imepoteza ladha yake, itakolezwaje? Basi haifai kitu ila kutupwa nje na kukanyagwa na watu. Ninyi ni nuru ya ulimwengu. Mji ulio juu ya mlima hauwezi kusitirika"*** (Mathayo 5:13-14).

Ninakusudia kuwa mwema na kutenda mema. ***"Kwa hiyo kadiri tupatavyo nafasi na tuwatendee watu wote mema, na hasa jamaa ya waaminio"*** (Wagalatia 6:10).

Ninakusudia kuwa jirani. ***"'Unadhani ni yupi kati ya hawa watatu aliyekuwa jirani yake yule aliyeangukia kati ya wanyang'anyi?' Naye akasema, 'Ni yule aliyemwonea huruma.' Ndipo Yesu akamwambia, 'Nenda ukafanye vivyo hivyo.'"*** ( Luka 10 :36-37).

Ninakusudia kuonesha rehema, na neema. ***"Heri wenye rehema, maana hao watapata rehema"*** (Mathayo 5:7).

Hatuna njia ya kujua mapambano wanayowakabili wengine, lakini tunaweza kuonyesha upendo wa Mungu, huruma ya Kristo na moyo wa mtumishi.

Siku zote nitakuwa na shukrani kwa ajili ya mwanangu, kwa ajili ya mtu alikuwa na maisha aliishi. Ingawa alikufa, bado yu hai moyoni mwangu na katika ulimwengu wa nje.

Shukrani hunisaidia kukabiliana na kila siku, hunisaidia kushikilia mema ya maisha yake na mema ninayoweza kuwafanyia wengine.

Sio matembezi rahisi. Hapana, lakini ni takatifu.

Kwa hiyo, unawezaje kukabiliana na hasara yako, huzuni yako? Labda yako ni ya hali tofauti—kufiwa na mwenzi, mzazi, ndugu au rafiki. Au, pengine hasara yako si ya mtu fulani bali ya kitu fulani—afya, usalama au sehemu nyingine muhimu ya maisha yako.

Natamani ningekuwa na tiba ya kimiujiza ya kutoa, lakini hakuna mtu aliye nayo. Jibu pekee ni kuchukua siku moja, saa moja, dakika moja, kwa wakati mmoja, kufungua moyo wako kwa shukrani kwa mambo mazuri uliyo nayo na kuwa mfereji wa kushiriki na wengine. Huduma. Upendo. Ndivyo ilivyo. Hilo ndilo jibu pekee ambalo nimepata.

Sio nadharia tu. Kweli inasaidia.

Tumeambiwa hatutakuwa na zaidi cha kubeba kuliko tunavyoweza kushughulikia. ***"Jaribu halikuwapata ninyi, isipokuwa lililo kawaida ya wanadamu; lakini Mungu ni mwaminifu ambaye hatawaacha mjaribiwe kupita mwezavyo, lakini pamoja na lile jaribu atafanya na mlango wa kutokea, ili mweze kustahimili"*** (1 Wakorintho 10:13). Imekuwa vigumu kukubali hilo, na bado, bado ninaishi hapa. Ninaona kwamba Alex bado anashiriki sehemu maishani pia, kupitia mimi, na wengine wanaompenda. Bado ana ushawishi, bado anagusa mioyo, bado analeta tabasamu.

Kwa yeyote anayehangaika na huzuni, ningesema hivi: Msherehekeeni yule mnayemwomboleza; mkumbuke kwa ubora wake; mheshimu kwa zawadi zake; zungumza juu yake. Wapendwa walioondoka ni sehemu ya maisha yako, na watakuwa hivyo daima. Hadithi zao bado zina nguvu na kazi ya kufanya. Sasa, wewe ndiye mjumbe, mlinzi wa urithi wao, na utapata njia za kuwaacha watu unaowapenda na kuwakumbuka kumwagika katika maisha ya wengine kupitia wewe. Kuwa na shukrani walikuwa katika maisha yako ulikuwa na furaha nao. Una hiyo milele. Hakuna kitakachobadilisha hilo au kuandika upya historia hiyo. Kumbukumbu hizo na nyakati hizo ni zako, na hakuna kinachoweza kukuondolea hilo.

Sasa, wewe angalia mbele. Kila siku, kila usiku, hunileta karibu na kuona tena sura hiyo ninayoipenda. Uso wake ni mmoja wa wengi ninaowakumbuka, wale ambao tayari wako upande mwingine. Walakini, ninaamini itakuwa ya kwanza kuona nitakapojiunga nao.

Kwa hiyo, nasubiri, lakini nasubiri kwa amani. Huzuni ipo, ndiyo, ipo kila siku. Walakini, furaha kwamba aliishi, kwamba aligusa maisha mengi na maisha yake. Bado anafanya hivyo.

Ingawa ninaomboleza, ninafarijiwa. ***"Heri wenye huzuni, maana hao watafarijiwa"*** (Mathayo 5:4).

Ingawa mnaomboleza, mtafarijiwa.

Kulia ni kwa usiku, lakini furaha huja asubuhi. ***"Kwa maana hasira yake ni ya kitambo tu, Neema yake ni ya uzima; kilio kinaweza kukaa usiku kucha, lakini asubuhi huja furaha"*** (Zaburi 30:5).

Tuko usiku sasa, lakini alfajiri inakuja.

Ikifika, tutajua furaha, na kuungana tena. Vidonda vyetu vitapona, na mioyo yetu itakuwa mizima.

1 Wathesalonike 4:13-18

"Lakini, ndugu, hatutaki msijue habari zao waliolala mauti, msije mkahuzunika kama na wengine wasio na matumaini. Maana, ikiwa twaamini ya kwamba Yesu alikufa akafufuka, vivyo hivyo na hao waliolala katika Yesu, Mungu atawaleta pamoja naye. Kwa kuwa twawaambieni haya kwa neno la Bwana, kwamba sisi tulio hai, tutakaosalia hata wakati wa kuja kwake Bwana, hakika hatutawatangulia wao waliokwisha kulala mauti. Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu; nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza. Kisha sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani; na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele. Basi, farijianeni kwa maneno hayo."

# Ndoa Zisizo na Furaha Si Kosa la Mungu

Clarence Ravender

Ndoa si mpango wa kibinadamu, bali umewekwa na Mungu (Mwanzo 2:18, 24; Waebrania 13:4). Ni wajibu wa uaminifu, si tu kwa kila mmoja wao, bali pia kwa Mungu. Ni zaidi ya mkataba wa kisheria. Ni ushirikiano kati ya kila mmoja na mwingine na pamoja na Mungu. Ndoa ni muungano wa mwanaume na mwanamke wanaohitajiana. Sababu mojawapo inayofanya ndoa kuwa katika matatizo leo ni kwa sababu wengi wamepoteza hisia hii ya kuhitajika.

